BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Tano – Tarehe 19 Septemba, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2022/2023.

### Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2022/2023.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2022/2023.

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

25. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Bado suala la kutuwama kwa maji eneo la Zone “F” Mwanakwerekwe halijapatiwa ufumbuzi

    (a) Je, unafahamu kuwa watendaji wako walikwishatoa ahadi ya kufika katika eneo husika na kuzungumza na wananchi lakini ahadi hizo hawajazitekeleza hadi leo hii.

    (b) Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na tatizo la kutuwama maji eneo hilo na kutotekelezwa kwa ahadi walizozitoa watendaji wa Wizara hii.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

87. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Kwenye miaka ya 1990, tulishuhudia Benki yetu ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ikitoa huduma zake kwenye wilaya zetu. Kwa mfano, katika wilaya ya Micheweni PBZ walitoa huduma zao ndani ya Micheweni na baadae Konde na hata wilaya ya Wete. Hata hivyo, upatikanaji wa huduma hizo kupitia matawi ya PBZ hivi sasa umepungua badala ya kuongezeka.

    (a) Je, ni lini huduma za kibenki katika matawi zitarejea ndani ya wilaya ya Micheweni kama ilivyokuwa zamani.

    (b) Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya huduma hizi kuwafikia wananchi wilayani kwa kuwapunguzia masafa ya kuzifuata huduma hizo maeneo ya mjini pekee.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

71. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na utaratibu wa kuwakatisha njia wanafunzi wa skuli mbali mbali kwenye barabara kuu zinazopakana na maeneo ya skuli zao, utaratibu ambao pia huwa kwa vyuo na maeneo mengineyo. Kwa kawaida utaratibu huu huwekwa na wananchi wenyewe lakini hufanywa bila ya kufuata ipasavyo sheria za barabara.

Je, ni lini Serikali italiwekea utaratibu wa Kisheria suala hili.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

76. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli za Kiembesamaki Msingi “A” na “B” zina uhaba mkubwa wa vitendea kazi sambamba na uchakavu wa majengo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzipatia vitendea kazi skuli za Kiembesamaki Msingi “A” na “B”.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

31. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kipindi kirefu kukosekana kwa elimu ya afya ya udongo kumekuwa ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazowakabili wakulima wetu.

(a) Je, Wizara inashughulika vipi na tatizo hili.

(b) Je, ugawaji wa vifaa vya kupimia udongo utakidhi kiu ya kuwafikia wakulima wengi.

(c) Je, ni yepi matokeo ya majaribio ya vifaa vilivyotumika katika kuleta matokeo chanya.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

72. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumekuwa na changamoto kubwa na ya muda mrefu ya mripuko wa mara kwa mara kwa transforma iliyopo karibu na makaazi ya watu katika eneo la Kijichi mkabala na skuli ya 'Brilliant Academy'.

(a) Je, kwa kiwango gani Wizara yako inalifahamu tatizo hili.

(b) Ni lini Wizara yako itachukuwa hatua za kudumu za kulitatua tatizo hili, ili kuepusha athari zaidi zinazoweza kutokea hasa tukizingatia kwamba transforma hii ipo karibu sana na makaazi ya watu.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

Ripoti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2022/2023.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

Ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**19 Septemba, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**